HOTUBA YA MHE. PROF. IBRAHIM HAMIS JUMA,
JAJI MKUU WA TANZANIA SIKU YA UZINDUZI
WA WIKI YA SHERIA NCHINI
TAREHE 22 JANUARI, 2023 - DODOMA.

Mhe. Dkt. Philip Isidor Mpango**,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Dkt. Tulia Ackson (Mb), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Wahe. Majaji wa Mahakama ya Rufani,

Mhe. Khamis Ramadhan Abdallah, Jaji Mkuu wa Zanzibar,

Mhe. Mustapher Mohamed Siyani, Jaji Kiongozi,

Mhe.Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Waziri wa Katiba na Sheria,

Wahe. Majaji wa Mahakama Kuu,

Mhe. Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali,

Prof. Elisante Ole Gabriel, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania,

Mhe. Wilbert Martin Chuma, Msajili Mkuu wa Mahakama ya Tanzania

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika,

Wasajili, Wakurugenzi na Watendaji wa Mahakama,

Mahakimu na Mawakili,

Wageni waalikwa, Mabibi na Mabwana**.**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

1:0 UTANGULIZI:

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukamilisha matembezi ya kilomita **5** na kukutana hapa kwenye viwanja vya Mwalimu Nyerere katika maadhimisho ya Wiki ya Sheria yatakayohusisha elimu ya sheria kwa wananchi pamoja na maonesho ya shughuli mbalimbali za wadau wa sheria.

Aidha kwa namna ya kipekee nachukua nafasi hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kukubali mwaliko wangu kushiriki matembezi lakini pia kwa ajili ya kuzindua monesho ya wiki ya sheria.

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Pamoja na uwepo wa taarifa zinazohusu taratibu mbali mbali za Mahakama na utatuzi wa migogoro, wananchi walio wengi bado hawafahamu taratibu hizo na pia kuelewa ni namna gani sheria na taratibu zake zina uhusiano na uchumi au zinavyoweza kuathiri shughuli zao za kila siku za kijamii, kiuchumi, na uzalishaji mali.

Mahakama inafahamu kwamba sio wananchi wote tunaowahudumia wanafahamu vema haki na wajibu wao katika taratibu za kupata haki zao pale ambapo migogoro itaibuka

katika mahusiano yao ya kijamii au kiuchumi. Kwa sababu hiyo, Mahakama ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau wa utoaji haki kila mwaka hutumia maadhimisho ya wiki ya sheria kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi kufahamu taratibu mbalimbali za kupata haki na pia kuwaelimisha juu ya haki na wajibu wao katika kupata haki.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, wananchi wengi wanapozungumzia HAKI au HAKI itendeke, huwa na maana wapate USHINDI na wasiposhinda Haki huwa haijatendeka. Nakumbuka tarehe 29 Agosti, 2022 Ikulu Chamwino-Dodoma; wakati wa kuwaapisha Majaji wapya 21 na Kamishna Jenerali wa Magereza ulipewa nafasi ya kutoa Salamu. Nakumbuka ulitumia muda huo kuwakumbusha wananchi tafsiri ya HAKI, kuwa ni: **"Stahili ya mtu kwa mujibu wa Katiba au Sheria au Kanuni."** Wiki ya Sheria inapompa mwananchi elimu ya sheria, Kanuni na Taasisi zinazosimamia haki zake; unakuwa umemuwezesha mwananchi kuweza kuelewa stahiki zake zilizo ndani ya sheria na kutafuta njia za kuzipigania.

Kupitia maonesho haya ya WIKI YA SHERIA, wananchi watapata nafasi ya kufahamu Katiba, Sheria, Kanuni na taratibu

zinazohusu Haki na wajibu wao. Wananchi watapata nafasi ya kuona shughuli mbalimbali zinazofanywa na Mahakama na wadau wake katika kuboresha mazingira ya utoaji haki na pia kutoa mrejesho wa huduma wanazozipata kwa kutoa maoni yao.

Nawaomba wananchi waelewe kuwa ni mwananchi mwenyewe ndiye mwenye nafasi kubwa zaidi ya kujitafutia kwanza, taarifa muhimu kuhusu haki zake. Taarifa nyingi sana kuhusu Sheria, Kanuni na Taasisi zinazosimamia Haki zako zipo katika Tovuti za Taasisi za Umma. Jengeni tabia ya kujitafutia maarifa na ujuzi kwa kujisomea mengi yanayopatikana katika Tovuti za Taasisi katika mnyororo wa Haki. Silaha bora ya kupigania Haki ni kuelewa upatikanaji wa hiyo Haki unayopigania ipo chini ya Sheria, Kanuni au Taratibu ipi.

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Wiki ya sheria mwaka huu itaanza leo tarehe **22 Januari 2023** na kuendelea hadi tarehe **29/1/2023** na siku ya sheria itakuwa tarehe **1/02/2023** itakayofanyika hapa Dodoma na Mgeni Rasmi atakuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho ya wiki ya

sheria nchini kwa mwaka huu yataongozwa na kauli mbiu isemayo;

"UMUHIMU WA UTATUZI WA MIGOGORO KWA NJIA YA USULUHISHI KATIKA KUKUZA UCHUMI ENDELEVU: WAJIBU WA MAHAKAMA NA WADAU"

Utoaji elimu katika maadhimisho utakayoyazindua unatarajiwa kutolewa kwa namna mbalimbali ikiwemo vipindi vya redio, midahalo, na maonesho katika maeneo mbalimbali nchi nzima kwa kipindi chote cha maadhimisho. Lengo ni kuwafikia wananchi wengi hata wale wa vijijini kadri inavyowezekana. Natoa wito kwa wananchi kutumia fursa hii muhimu kwao kufuatilia elimu itakayotolewa.

2:0 SHUGHULI ZITAKAZOFANYIKA:

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Katika maadhimisho ya wiki ya sheria mwaka huu shughuli mbalimbali zimepangwa kufanyika ili kuboresha shughuli za utoaji haki.

2:1 Uzinduzi wa Kitabu Cha Miaka saba Kituo cha Usuluhishi.

Mwaka 2015 Mahakama ilianzisha kituo cha Usuluhishi cha Dar es Salaam kwa lengo la kusuluhisha mashauri ya madai yanayofunguliwa katika Mahakama Kuu kanda ya Dar es Salaam na Divisheni ya Ardhi.

Kitabu hiki kitasadia kuelezea mchango wa kituo hicho, mafanikio na uzoefu uliopatikana katika matumizi ya njia hii mbadala ya utatuzi wa migogoro. Hivyo naomba wadau na wananchi wote kujisomea kitabu hicho ili mpate uelewa mpana kuhusu kituo hiki cha usuluhishi na faida zake katika kutatua migogoro yetu.

2:2 Uzinduzi wa Majengo manne ya Mahakama za Wilaya

Tarehe 25 Januari 2023 Mahakama inatarajia kuzindua majengo ya Mahakama za Wilaya ya Manyoni Mkoani Singida. Bunda Mkoani Mara, Rungwe mkoani Mbeya na Sikonge mkoani Tabora. Uzinduzi wa majengo hayo ni mwendelezo wa jitihada za Mahakama kuboresha miundombinu na mazingira ya utoaji haki na katimaye kupunguza mlundikano wa mashauri.

Imani ya Mahakama ni kwamba miundo mbinu mizuri na huduma nzuri inaweza kubadili mitizamo ya wananchi na kuongeza pia imani kwa mfumo wa utoaji haki na kudumisha amani na utulivu, jambo ambalo ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa wananchi yetu.

3: TEHAMA, TEHAMA, TEHAMA

Mheshimiwa Makamu wa Rais, Karne ya 21 shughuli za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii ni kupitia TEHAMA, TEHAMA, TEHAMA.

Mwaka jana katika maadhimisho kama haya nilieleza kwamba Mahakama na wadau wake hawawezi kubaki nyuma kwenye hizi zama za Mapinduzi ya Nne ya Viwanda ambapo matumizi ya TEHAMA yameshamiri.

Napenda kukuahidi kuwa Mahakama ya Tanzania ipo sambamba na Programu ya Serikali ya Tanzania ya kufikia TANZANIA YA KIDIJITALI. Mahakama ya Tanzania itaendelea na jitihada za dhati katika kutekeleza wajibu wetu wa kikatiba wa utoaji haki kwa kutumia mbinu mbalimbali kama matumizi ya

TEHAMA na *Artificial Intelligence* ili kurahisisha na kuharakisha zoezi hilo la utoaji haki.

Mahakama haiwezi kubaki nyuma wakati wananchi wameyakubali na kuyaishi Mapinduzi yas Nne ya Viwanda. Wananchi wengi wanafanya shughuli zao za kiuchumi zikiwemo biashara kwenye mitandao, matangazo na mauzo ya bidhaa kwenye mitandao. Miamala kupitia simu, Mabenki, Taasisi za Kifedha tayari ni sehemu ya Maisha ya kiuchumi na kijamii kwa Watanzania. Aidha tunaishi pia kwenye zama ambazo Sheria na Utoaji wa Haki inafanyika kupitia kwenye mitandao na huduma nyingi kuhusu masuala ya haki hupatikana na kutolewa bila ya kuonana ana kwa ana.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, maneno DIGITAL DIVIDE imetafsiriwa kuwa ni utofauti katika matumizi ya TEKNOLOJIA unaowatenganisha wale wenye uwezo wa kupata kwa urahisi huduma za kimtandao, na wale ambao hawana uwezo huu. Unawatenganisha wale wenye ujuzi wa kutumia mifumo ya kidijitali na wale ambao hawana ujuzi wowote. Sisi Mahakama tumetayarisha Mtaala wa kuwapa watumishi wote ujuzi wa kufanya kazi na kutoa huduma kwa njia ya kidijitali. Katika

Karne hii ya 21, uwezo mdogo katika matumizi ya TEHAMA unaweza kuwa chanzo cha utofauti kati ya wenye uwezo na wasio na uwezo au hata kati ya wanaume na wanawake katika kupata taarifa muhimu za kisheria na kimahakama kupitia mifumo ya TEHAMA.

Ni muhimu wananchi wafahamu pia namna ambavyo migogoro ya biashara, kazi au mikataba inayoweza kutokea kwa njia za mitandao; na inavyoweza kutatuliwa (ikiwemo kwa njia ya usuluhishi) kwa njia ya TEHAMA.

Mwandishi mmoja wa Uingereza Bwana **Richard Susskind** katika kitabu chake kiitwacho—MAHAKAMA MTANDAO NA HATIMA YA UTOAJI HAKI **(ONLINE COURTS, AND FUTURE OF JUSTICE, *OXFORD UNIVERSITY PRESS (2019)*** ameeleza, ukurasa wa 138, namna ambavyo mitandao ya mawasiliano ikiwemo barua pepe, imeweza pia kutumika katika kutatua migogoro, ikiwemo pia kwa njia ya usuluhishi; bila ya wahusika na migogoro kulazimika kukutana ana kwa ana na hivyo kuokoa muda na fedha. Alisema kuwa ipo mifano ya barua-pepe na majadiliano kupitia mitandao inavyoweza kutatua migogoro kwa

njia inayoitwa majadiliano-kimtandao *(e-negotiation)* au usuluhishi-mtandao *(e-mediation)* unaotumia wasuluhishi kusaidia kutatua migogoro. Njia zote hizi za utatuzi wa migogoro imewezekana bila ya wahusika kukutana katika chumba au mahakamani.

Rai yangu ni kwamba wananchi ambao wanao uwezo wa kutumia TEHAMA kwa miundombinu rahisi ikiwemo simu janja, tusibaki nyuma. Tembeleeni Mabanda ya Maonesho ya Mahakama mtaona dunia ya kidijitali ambayo Mahakama inaelekea. Tutumie nafasi hiyo kwa kujisomea taarifa, taratibu, miongozo na maamuzi mbali mbali yanayohusu haki na wajibu wao katika shughuli za kiuchumi zikiwemo biashara na namna ya kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi.

Aidha natoa rai kwa wadau wa sheria watakaotoa elimu kwa wananchi nao kuzielewa zama hizi na mazingira ambayo wananchi wanafanya shughuli zao za kiuchumi. Katika zama hizi za utandawazi, kuna ushindani na matumizi makubwa ya teknolojia katika shughuli za kiuchumi na biashara. Kwa sababu hiyo Wadau wa sheria wakiwemo mawakili ni muhimu kubadilli fikra na kujiongezea maarifa ya

utatuzi wa migogoro kwa usuluhishi ikiwemo ya kibiashara au kazi zinazofanyika kwenye mitandao.

Kwa mawakili wasomi, narejea ushauri wangu kwao nilioutoa tarehe **8/7/2022** wakati nikiwapokea na kuwakubali mawakili wapya **335** walioorodheshwa kwenye daftari la mawakili- Dar es Salaam kwamba upo umuhimu wa mawakili kujitayarisha kufanya kazi za Waendesha Maridhiano, Majadiliano, Upatanishi na Usuluhishi (**Reconciliation, Negotiation, Mediation and Arbitration)** kwa faida ya biashara na uwekezaji wa ndani na wa kutoka nje ya Tanzania.

Mahakama itaendea kutekeleza jukumu lake la kuhimiza usuluhishi baina ya wadau na kuweka taratibu zitakazowezesha usuluhishi kulingana na mahitaji hii ni pamoja na matumizi ya TEHAMA. Hii itasadia kukidhi ushindani wa uchumi wa sasa wa kikanda na dunia.

Mheshimiwa Makamu wa Rais,

Wiki hii ya Sheria inahimiza migogoro ikamilike kwa haraka kwa njia ya USULUHISHI. Pengine wananchi wengi hawafahamu kwamba mashauri yanayofunguliwa mahakamani, wakati mwingine hutokana na wadaawa kukosa utayari wa

kuzungumza baina yao na wakati mwingine kudhani kila wakati ni lazima mshindi apatikane.

Utatuzi wa migogoro ya ardhi na ndoa na hata mashitaka madogo ya jinai taratibu zinaruhusu na kuhimiza kupitia taratibu za usuluhishi. Kwa wananchi wanaweza kutumia zaidi fursa ya za uwepo wa mitandao ya mawasiliano na mitandao ya kijamii kutafuta usuluhishi wa maswala yanayoweza kumalizika kwa njia ya majadiliano. Nawaasa wananchi kufika kwenye maonesho haya na kujielimisha na watakaopata elimu wawe chachu kwa wengine.

Endapo wananchi watakuwa mstari wa mbele kuwa tayari kutatua migogoro kwa njia ya usuluhishi kutawapa nafasi ya kufanya shughuli za uzalishaji na kujiongezea kipato na kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Makamu wa Rais, Kwa mara nyingine nakushuru kwa kukubali kuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Wiki ya Sheria na kushiriki nasi katika shughuli za leo. Kwa heshima naomba sasa kukukaribisha utupatie nasaha zako na hatimaye uzindue maadhimisho ya Wiki ya Sheria 2023.

Mheshimiwa Makamu wa Rais Karibu sana.